# HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE

## MUHTASARI WA KIKAO MAALUM CHA KAMATI YA FEDHA NA UONGOZI KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA IDD NYUNDO TAREHE 28/10/2021

## 1.0 WALIOHUDHURIA

### 1.1 WAJUMBE

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Abdallah Said Mtinika | - | Diwani Kata ya Kibondemaji (Mstahiki Meya) | - | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Arnold Emmanuel Peter | - | Diwani Kata ya Kurasini (Naibu Meya) | - | Mjumbe |
| 3. | Mhe. Juma R. Mkenga | - | Diwani Kata ya Miburani | - | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Mariam Juma Mtemvu | - | Diwani Viti Maalum | - | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Caroline David Henrich | - | Diwani Viti Maalum | - | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Twahil Shabani Kamona | - | Diwani Kata ya Charambe | - | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Said Hassan Fella | - | Diwani Kata ya Kilungule | - | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Amiri Bakari Salum | - | Diwani Kata ya Kilakala | - | Mjumbe |
| 9. | Mhe. Morrice E. Kapinga | - | Diwani Kata ya Makangarawe | - | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Abdallah J. Chaurembo | - | M/Jimbo la Mbagala | - | Mjumbe |
| 11. | Mhe. Doroth G. Kilave | - | M/Jimbo la Temeke | - | Mjumbe |
| 12. | Mhe. Janejelly J. Ntate | - | M/Viti Maalum | - | Mjumbe |
| 13. | Mhe. Dr. Paulina Nahato | - | M/Viti Maalum | - | Mjumbe |
| 14. | Mhe. Christopher Kabalika Mwansasu | - | Diwani Kata ya Sandali | - | Mjumbe |
| 15. | Mhe. Fatuma Michael Shija | - | Diwani Kata ya Kiburugwa | - | Mjumbe |
| 16. | Mhe. Abdallah Mzee Bwera | - | Diwani Kata ya Mianzini | - | Mjumbe |
| 17. | Mhe. Mwadunia Ramadhani Zame | - | Diwani Viti Maalum | - | Mjumbe |
| 18. | Mhe. Athumani Jumanne Nyamlani | - | Duwabu Kata ya Kijichi | - | Mjumbe |
| 19. | Mhe. Mohamed Selemani Mketo | - | Diwani Kata ya Toangoma | - | Mjumbe |
| 20. | Mhe. Kevin Abiud Mhidze | - | Diwani Kata ya Chang'ombe | - | Mjumbe |
| 21. | Bw. Elihuruma Mabelya | - | Mkurugenzi wa Manispaa Temeke | - | Katibu |

### 1.2. WATENDAJI

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Bw. Mrisho A.Mlela | - | Mkuu wa Idara ya Utawala na Utumishi |
| 2. | Bibi. Veronica Igoko | - | Kaimu Mkuu wa Idara ya Ardhi, Maendeleo na Makazi |
| 3. | Dr. Gwamaka Mwabulambo | - | Mkuu wa Idara ya Afya |
| 4. | Dkt. Janeth Barongo | - | Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari |
| 5. | Bibi. Miriam Marwa | - | Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi |
| 6. | Bibi. Elde Kimaro | - | Mkuu wa Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika |
| 7. | Bibi. Rose Mwaita | - | Mchumi |
| 8. | Bw. Ally Hatibu | - | Mkuu wa Idara ya Usafishaji na Mazinigira |
| 9. | Bibi. Davina Majinge | - | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA |
| 10. | Bw. Twahir Makwega | - | Afisa Ugavi na Manunuzi |
| 11. | Bibi Glory Kessy | - | Mhasibu wa Mapato |
| 12. | Bibi. Elizabeth Mdalagwila | - | Mtakwimu |
| 13. | Bibi. Judith Maziwa | - | Kaimu Mkuu wa kitengo cha Ukaguzi wa Ndani |
| 14. | Bw. Patrick Mchomba | - | Kaimu Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara |
| 15. | Bibi. Herieth Makombe | - | Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii na Vijana |
| 16. | Bw. Sosthenes Chacha | - | Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi na Ugavi |
| 17. | Eng.Juma Magotto | - | Mkuu wa Idara ya Ujenzi |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 18. | Bw. Mgaya Mtundu | - | Mkuu wa Kitengo cha Nyuki |
| 19. | Bibi. Delphina Wambura | - | Mkuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvi |
| 20. | Bibi. Honorina Mkunda | - | Kaimu Mkuu wa Idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji |
| 21. | Bibi. Aimbora Nnko | - | Mkuu wa Kitengo cha Uchaguzi |
| 22. | Bibi. Annette Kisamo | - | Mratibu Msaidizi wa Mradi wa DMDP |
| 23. | ACP Andrew M. Mchome | - | Askari Polisi |

**1.4 WAALIKWA:**

| | | |
|---|---|---|
| 1.Bw. Mafuku R.Kabeya | - | Kaimu Katibu Tawala |
| 2. Bw. Sadath Mtware | - | Afisa Tarafa Chang'ombe |
| 3. Bibi. Theodora Malata | - | Kaimu Afisa Tarafa Mbagala |

**1.5 SEKRETARIETI**

| | | |
|---|---|---|
| 1. Bibi. Juliana Zacharia | - | Mwandishi wa Mikutano |
| 2. Bibi. Lucy Kiyungu | - | Mwandishi wa Mikutano |
| 3. Bw. Adinani Bilali | - | Mwandishi wa Mikutano |

**2.0 MUHT. NA. TEM/6/10/2021: KUFUNGUA KIKAO**

Mwenyekiti alifungua kikao saa 7.30 mchana.

**3.0 MUHT. NA. TEM/7/10/2021: KUTHIBITISHA AGENDA**

Katibu aliwasilisha agenda zifuatazo kwa ajili ya majadiliano

1. Kufungua kikao.
2. Kuthibitisha agenda.
3. Taarifa ya Mapokezi ya Fedha Tsh.3,440,000,000 na Miradi itakayotekelezwa kupitia mpango wa Maendeleo ya Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO - 19
4. Maombi ya kuhamisha Fedha za ujenzi wa vyumba vya madarasa 36 zilizopokelewa katika shule ambazo hazina maeneo ya kujenga.
5. Kufunga kikao.

**4.0 MUHT. NA.TEM/8/10/2021: TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA TSH. 3,440,000,000.00 NA MIRADI ITAKAYOTEKELEZWA KUPITIA MPANGO WA MAENDELEO YA USTAWI WA TAIFA NA MAPAMBANO DHIDI YA UVIKO-19**

Kaimu Mkuu wa Idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji, akiwasilisha taarifa hiyo alieleza kuwa Halmashauri ya Manispaa ya Temeke imepokea fedha Tsh. **3,440,000,000.00** kutoka kwa Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ajili ya kuboresha Miundombinu ya Elimu na Afya (Sekta ya Elimu Sekondari na Sekta ya Afya). Fedha hizi zimeelekezwa kwenye maeneo ya vipaumbele vinavyogusa wananchi moja kwa moja kwa ajili ya kuwaondolea kero katika kuzifikia na kuzipata huduma za Afya na Elimu katika Manispaa ya Temeke.

Aidha, Halmashari ya Manispaa ya Temeke kama zilivyo Halmashauri nyingine Tanzania itapokea fedha kwa ajili ya kuboresha miundombinu na mazingira ya kufanyia biashara kwa wafanyabiashara wadogo.

***Miradi itakayotekelezwa kutokana na fedha za Mpango wa Maendeleo Ya Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO-19***

| NA. | MRADI | IDADI | KIASI CHA FEDHA |
|---|---|---|---|
| 1. | Ujenzi wa vyumba vya madarasa ya shule za sekondari | 157 | 3,140,000,000.00 |
| 2. | Ujenzi wa jengo la huduma ya Dharura (EMD) | 1 | 300,000,000.00 |
| | **JUMLA KUU** | | **3,440,000,000.00** |

**MJADALA:**
Mhe. Said Hassan Fella alitoa hoja ya kupokea taarifa hiyo iweze kujadiliwa.

Mhe. Amiri Bakari Salum aliunga mkono hoja hiyo.

Mhe. Mohamed Selemani Mketo alitaka kujua eneo litakalotumika kujenga jengo la huduma ya Dharula (EDM).

Mkuu wa Idara ya Afya alieleza kuwa ujenzi wa jengo la huduma ya dharula utafanyika katika kituo cha Afya cha Yombo Vituka.

Wajumbe walipokea taarifa hiyo na kuithibitisha.

**AZIMIO:**
Kikao kiliridhia na kupitisha taarifa ya mapokezi ya fedha na miradi itakayotekelezwa kupitia mpango wa maendeleo ya Ustawi wa Taifa na mapambano dhidi ya UVIKO – 19.

**5.0 MUHT. NA.TEM/9/10/2021: MAOMBI YA KUHAMISHA FEDHA ZA UJENZI WA VYUMBA VYA MADARASA 36 ZILIZOPOKELEWA KATIKA SHULE AMBAZO HAZINA MAENEO YA KUJENGA**

Kaimu Mkuu wa Idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji akiwasilisha Taarifa hiyo alieleza kuwa Halmashauri ya Manispaa ya Temeke imepokea fedha **Tsh. 3,140,000,000.00** kwa ajili ya ujenzi wa vyumba **157** vya madarasa chini ya Mpango wa maendeleo kwa ustawi wa Taifa na mapambano dhidi ya UVIKO – 19 fedha hizi zimeingizwa katika akaunti za Shule **30** kulingana na mgawanyo wa vyumba vya madarasa.

Pamoja na mapokezi ya fedha hizo kuna Shule **11** za Barabara ya Mwinyi, Buza, Chang'ombe, Keko, Kichanga, Lumo, Pendamoyo, Relini, Tandika, Temeke na Wailes hazina maeneo ya kujenga nyumba vilivyopangwa hivyo kulazimika kuhamisha fedha hizo na kuzipeleka katika Shule za Kijichi, Taifa,

Toangoma, Malela na kuanzisha ujenzi wa Shule mpya katika eneo la Dovya – Chamazi.

Pamoja na ombi hili naambatanisha na jedwali linaloonyesha maombi ya kuhamisha maeneo ya ujenzi wa madarasa 36.

## HALI YA UPUNGUFU WA VYUMBA VYA MADARASA KWA KIDATO CHA KWANZA 2022

| NA. | HALMASHAURI | JIMBO LA UCHAGUZI | KATA | JINA LA SHULE | UPUNGUFU WA VYUMBA VYA MADARASA (UWIANO 1:50) | KIASI CHA FEDHA KILICHOLETWA | IDADI YA VYUMBA KUTOKANA NA FEDHA | TOFAUTI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Temeke Manispaa | TEMEKE | Kilakala | Barabara ya Mwinyi | | 80,000,000.00 | 4 | 4 |
| 2. | Temeke Manispaa | TEMEKE | Buza | Buza | | 80,000,000.00 | 4 | 4 |
| 3. | Temeke Manispaa | MBAGALA | Chamazi | Chamazi | 2 | 40,000,000.00 | 2 | 0 |
| 4. | Temeke Manispaa | MBAGALA | Toangoma | Changanyikeni | 2 | 40,000,000.00 | 2 | 0 |
| 5. | Temeke Manispaa | TEMEKE | Miburani | Chang'ombe | | 80,000,000.00 | 4 | 4 |
| 6. | Temeke Manispaa | MBAGALA | Mianzini | Charambe | 4 | 80,000,000.00 | 4 | 0 |
| 7. | Temeke Manispaa | TEMEKE | Kurasini | Diplomasia | 12 | 240,000,000.00 | 12 | 0 |
| 8. | Temeke Manispaa | TEMEKE | Temeke | Karibuni | 7 | 140,000,000.00 | 7 | 0 |
| 9. | Temeke Manispaa | TEMEKE | Keko | Keko | 1 | 80,000,000.00 | 4 | 3 |
| 10. | Temeke Manispaa | TEMEKE | Miburani | Kibasila | | | 0 | 0 |
| 11. | Temeke Manispaa | TEMEKE | Miburani | Kibasila 'B' | 7 | 140,000,000.00 | 7 | 0 |
| 12. | Temeke Manispaa | TEMEKE | Azimio | Kichangani | 1 | 80,000,000.00 | 4 | 3 |
| 13. | Temeke Manispaa | MBAGALA | Kijichi | Kijichi | 6 | 120,000,000.00 | 6 | 0 |
| 14. | Temeke Manispaa | MBAGALA | Kiburugwa | Kingugi | | | 0 | 0 |
| 15. | Temeke Manispaa | TEMEKE | Kurasini | Kurasini | 13 | 260,000,000.00 | 13 | 0 |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 16. | Temeke Manispaa | TEMEKE | Yombo Vituka | Lumo | 1 | 80,000,000.00 | 4 | 3 |
| 17. | Temeke Manispaa | MBAGALA | Toangoma | Malela | 6 | 120,000,000.00 | 6 | 0 |
| 18. | Temeke Manispaa | MBAGALA | Mbagala Kuu | Mbagala | 2 | 40,000,000.00 | 2 | 0 |
| 19. | Temeke Manispaa | MBAGALA | Mbagala Kuu | Mbagala Kuu | 4 | 80,000,000.00 | 4 | 0 |
| 20. | Temeke Manispaa | MBAGALA | Chamazi | Mbande | 4 | 80,000,000.00 | 4 | 0 |
| 21. | Temeke Manispaa | TEMEKE | Miburani | Miburani | 7 | 140,000,000.00 | 7 | 0 |
| 22. | Temeke Manispaa | MBAGALA | Toangoma | Mikwambe | 6 | 120,000,000.00 | 6 | 0 |
| 23. | Temeke Manispaa | TEMEKE | Temeke | Ndalala | 9 | 180,000,000.00 | 9 | 0 |
| 24. | Temeke Manispaa | MBAGALA | Charambe | Nzasa | 5 | 100,000,000.00 | 5 | 0 |
| 25. | Temeke Manispaa | TEMEKE | Temeke | Penda Moyo | | 80,000,000.00 | 4 | 4 |
| 26. | Temeke Manispaa | TEMEKE | Mtoni | Relini | 2 | 80,000,000.00 | 4 | 2 |
| 27. | Temeke Manispaa | MBAGALA | Chamazi | Saku | 4 | 80,000,000.00 | 4 | 0 |
| 28. | Temeke Manispaa | TEMEKE | Tandika | Tandika | 3 | 80,000,000.00 | 4 | 1 |
| 29. | Temeke Manispaa | TEMEKE | Sandali | Temeke | | 80,000,000.00 | 4 | 4 |
| 30. | Temeke Manispaa | MBAGALA | Toangoma | Toangoma | 8 | 160,000,000.00 | 8 | 0 |
| 31. | Temeke Manispaa | TEMEKE | Kurasini | Uhamiaji | 5 | 100,000,000.00 | 5 | 0 |
| 32. | Temeke Manispaa | TEMEKE | Miburani | Wailesi | | 80,000,000.00 | 4 | 4 |
| | | | **JUMLA** | | **121** | **3,140,000,000.00** | **157** | **36** |

**MJADALA:**
Mhe. Mariam Juma Mtemvu alitoa hoja ya kupokea taarifa hiyo iweze kujadiliwa.

Mhe. Kevin Abiud Mhidze aliunga mkono hoja.

Mhe. Said Hassan Fella alieleza kuwa Serikali ilitoa maelezo kuwa fedha za UVIKO-19 zitafika kwenye kila eneo la Halmashauri, Lakini zipo baadhi ya kata ambazo hazina Sekondari ikiwemo ya Kilungule, Hivyo akapendekeza fedha hizo zielekezwe kujenga Shule ya Sekondari kwenye kata hizo.

Mhe. Amiri Bakari Salimu aliunga mkono hoja ya mjumbe, Aidha aliongeza kuwa msongamano wa wanafunzi katika Shule ya Sekondari barabara ya Mwinyi umetokana na wanafunzi wanaotoka Kata ya Makangarawe, hivyo akashauri kujengwa shule katika kata hiyo.

Mhe. Christopher Kabalika Mwansasu aliunga mkono hoja ya wajumbe waliochangia awali, aliongeza kuwa pamoja na uwepo wa baadhi ya Kata kukosa maeneo ya kujenga madarasa na kupelekea kukosa fedha za ujenzi lakini zina madarasa mabovu ambayo yanaweza kufanyiwa ukarabati na kutumika.

Katibu alieleza kuwa fedha zilizoletwa zina maelekezo ambayo hayaruhusu kufanya ukabarati wa madarasa, hata hivyo akashauri hayo madarasa mabovu yatakarabatiwa kwa kutumia fedha za mapato ya ndani ya Halamshauri.

Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari alifafanua na kueleza kuwa, zipo Kata tano ambazo hazina Sekondari kwa kukosa maeneo ya ujenzi au kuwa na maeneo yenye ukubwa usiotosheleza, akaongeza kuwa Halmashauri iko kwenye mchakato wa kupata na kuongeza maeneo kwenye Kata hizo. Hivyo kutokana na kutokamilika mchakato wa kupata maeneo na uharaka wa kutekeleza mradi wa ujenzi wa madarasa imeshindikana kupeleka fedha za ujenzi wa madarasa kwenye Kata hizo. Aidha aliwahakikishia wajumbe kuwa Halmashauri itajenga shule kwenye Kata ambazo hazina Sekondari baada ya kukamilika mchakato wa kupata maeneo ya kujenga.

Mhe. Mohamed Selemani Mketo alikiri kuridhishwa na ufafanuzi uliotolewa na kusema kuwa kwa vile matumizi ya fedha hizo yamewekewa muda maalum ambao ni mchache, kamati ipitishe na kuweka mkakati wa kujenga sekondari kwenye kata ambazo hakuna Shule za Sekondari kwenye bajeti zijazo za Halmashauri.

Wajumbe walipokea taarifa hiyo na kuridhia.

**AZIMIO:**
Kikao kiliridhia na kupitisha Maombi ya kuhamisha Fedha za ujenzi wa vyumba vya madarasa 36 zilizopokelewa katika shule ambazo hazina maeneo ya kujenga.

**6.0 MUHT. NA.TEM/10/10/2021: KUFUNGA KIKAO**
Kabla ya kufunga kikao Naibu Meya alisisitiza haja ya kufanya maandalizi mazuri na mapema ya taarifa za vikao ili kufanya vikao vya Kamati kwa kufuata matakwa ya kanuni za Halmashauri na ratiba ya vikao iliyopitishwa na wajumbe.

Mwenyekiti alifunga kikao saa 9.00 Alasiri.

..............................
**MWENYEKITI**

..............................
**KATIBU**

**UMETHIBITISHWA**
**TAREHE** ...8/11/2021